

Thief in the Night
Study on the Rapture
By Frank DiMora

# MWIZI AJAYE USIKU

# IMEANDIKWA NA FRANK DIMORA

# Agosti 7,2011

Kwa nini Yesu anataka tuwe macho kuhusiana na Kalenda ya bibilia? Yesu anataka wanaotazamia kurudi kwake kuwa tayari wakati ajapo kuchukua kanisa kutoka ulimwengu. Njia ya pekee mtu anaweza fanya hivyo nikujua nini anatazamia. Niwazi kama mchana ninini wakristo wanatazamia, lakini ningesema wakristo hawana dokezo ya ni nini ishara. Kwanini hawajui? Naweza ona sababu mbili. Kwanza; wako katika kanisa ampapo mchungaji hafunzi kuhusu ishara za nyakati. Pili, wakristo hawasomi neno wenyewe na hivyo hawajui ishara. Wacha nikusaidie kuelewa ujumbe muhimu kutoka kwa Kristo. Ikiwa utaelewa ni nini Kristo alikuwa akiongea kuhusu, itakuwa wazi kwako na familia mnachopaswa kuwa mkitazamia.

Watu wengi wameniuliza kwa nini upoteze muda mwingi kujua ni lini Yesu atarudi tena, Yesu mwenyewe alisema kuwa hakuna mtu ajuaye. Wacha ni mnuku Yesu katika Mathayo 24:36 ili ujuwe kile ninacho zungumza kuhusu. **36"Hakuna ajuaye siku wala saa, hata malaika mbinguni hawajui wala Mwana, ila Baba peke yake"**. Sasa ningependa utambue kile ambacho Yesu anasema kuhusiana na mawazo ya wayahudi na tamaduni zao. Msomo yakuwa hiyo siku na saa hakuna ajuaye mtu, ni msemo wakawaida katika semi za waibrania ya sikukuu ya Rosh hashanah. Rosh hashanah ni moja wapo ya sikukuu saba za wayahudi. Nainajulikana kwa wayahudi kama sikuku ya tarumbeta. Sikuku ya tarumbeta hufanyika katika ulingo Katika Mambo ya Walawii 23 unaona sikukuu hizi na majira mahsusi iliyo wekwa wazi katika marudio ya kila mwaka yaliyo fundisha kwa kihistoria na kiunabii mpango mzima wa Mungu. Mpango huu ulihusisha kukuja kwa kristo na vile Kristo ataleta ukombozi kwa wote watakao mpokea. Kwa ufupi, Mungu ametupatia kalenda ya kibibilia. Kutokana na sikukuu saba za kibibilia zile zilizo salia kutimika ni sikuku ya mwanguko ambayo ni Rosh hashanah ambayo pia huitwa sikukuu ya tarumbeta, Yom kippur, ambayo ni siku ya kuondolewa dhambi, an hema ya bwana. Naenda kutilia mkazo sikukuu ya tarumbeta kwa sababu kulingana na kalenda ya Mungu, hii ndiyo inafuatilia kutimika kwa huo mfwatilio. Kutambua huu ujumbe wacha nirejelee maneno aliyosema Yesu Kristo katika Mathayo 24:26 Wakati alisema " Hakuna mtu ajuaye siku wala saa." Huu mtari unahusiana na harusi ya kiyahudi. Ilimlazimu baba kuhakikisha kuwa mwanawe alikuwa ametayarisha kila kitu kwa ajili ya harusi. Kama mtu yeyote angemuuliza mvulana wa Kiyahudi ni lini siku ya harusi, angejibu "Muulize babangu ni yeye tuu ajuaye." Huu ulikuwa mtindo wa kawaida kwa wayahudi. Huu msemo ulikuwa jibu la kitamaduni. Wakati mda ulipo wadia wa harusi kufanyika, yule mvulana alitoka nje usiku wa manane na kupuliza tarumbeta ili kumjulisha bibi harusi kuwa amjia. Sikukuu ya tarumbeta ama Rosh Hashanah inahashiria kuwa hakikisho ya kitamaduni kuwa Rosh Hashanah itakuwa ndio wakati uliochaguliwa kwa unyakuzi wa

kanisa. Kama thibitisho ya haya, wacha nikuonyeshe yaliyo tendeka kwa harusi ya kiyahudi kuhusiana na Yesu Kristo na bii harusi wake, Kanisa.

Katika harusi ya kiyahudi, msichana myahudi huonyesha kuwa ataoleka naye kwa kukubali posa kwa kunywa kikombe cha divai anacho mpokeza. Ni nini Yesu alicho fanya katika karamu ya Meza ya Bwana? Yesu alipitisha kikombe cha divai na walio pokea divai na kunywa walikubali kuwa bii harusi wake. Pili, mvulana myahudi alilazimika kulipa mahari kwa wazazi wa bii harusi. Ni nini Yesu alicho fanya, na nini ilikuwa dhamana aliyo lipa? Yesu alilipa garama kwetu kama bii harusi wake kwa maisha yake kwa kufa msalabani kwa ajili yetu. Jambo lingine walilo fanya wavulana wayahudi ili kutayarisha harusi, ilikuwa kumpa bii harusi zawadi. Nizawadi gani Yesu alimpa bii harusi wake Kanisa? Yesu alitupa zawadi ya roho mtakatifu.

Jambo lingine ambalo mvulana myahudi alipaswa kufanya ili kutayarish kwaajili ya harusi ilikua kwenda kuandaa makao ya kuishi yeye na mkewe watakapo oana. Je unakumbuka maneno ya Yesu Kriso katika Yohana 14:3? Yesu alisema. "Na kama nikienda kuwaandalia makao, nitarudi nakuwachukua ili nilipo nanyi muwepo." Hapa ndipo Yesu alipo sasa. Anaandaa makao kwa kanisa ambalo ni bii harusi wake. Jambo lingine ambalo mvulana myahudi alipaswa kufanya ili kuandaa kwa harusi ya kiyahudi ni hili. Angalichukua umati wa watu pamoja naye usiku wa manane na kwenda nje na kupuliza tarumbeta (Shofar) kwa ajili ya bii harusi wake. Shofar ni upembe. Soma kile ambacho Yesu alimwambia Paulo aandike katika 1.Wathesalonike 4:15-16.

Paulo anataja wakati timilifu wa matukio haya mara mbili! Katika mstari wa kumi na tano anasema hii hufanyika wakati wa kurudi kwa Bwana na mstari wa kumi na sita, Yesu anashuka kutoka mbinguni na mwito mkuu na sauti wa malaika mkuu na tarumbeta ya Mungu. Hapa ndipo Yesu atakapo tujia sisi kanisa kama vile Kijana Myahudi angeweza kwanda usiku wa manane na kumuita mchumba wake. Hili ndilo litakua jambo lingine katika kalenda ya Mungu wakati wa sikukuu ya tarumbeta.

Jambo lingine ambalo lingalifanyika wakati wa harusi ya kiyahudi ambalo lilitukia wakati mvulana aliende nje kumchukua mchumba wake lilikua kwenda kukaa siku saba na mchumba wake ili kutekeleza ndoa katika chumba chao cha harusi. Wakati Yesu anakujia mchumba wake Kanisa, anachukua kanisa mbinguni kwa mwika saba. Kama ukitambua huu ndio wakati wa mwika saba ya dhiki. Skiza inavyo sema katika Isaiah 26:20-21 Kuhusiana na vyumba hivi. **20Nendeni, watu wangu, ingieni vyumbani mwenu na mfunge milango nyuma yenu, jificheni kwa kitambo kidogo mpaka ghadhabu yake ipite.**
**21Tazama, BWANA anakuja kutoka katika makao yake ili kuwaadhibu watu wa dunia kwa ajili ya dhambi zao. Dunia itadhihirisha umwagaji damu juu yake, wala haitaendelea kuwaficha watu wake waliouawa.**
Hivi ndivyo vyumba ambavyo Yesu ataweka Kanisa ndani kwa miaka saba ya dhiki ambayo itakumba ulimwengu. Kanisa mchumba wa Kristo, atafichwa kutokana na nyakati ngumu ambazo zitakumba ulimwengu wakati wa dhiki.

Kama uonavyo sasa kila kitu Yesu amefanya kulingana na tamaduni ya harusi za kiyahudi ambayo pia inazingatia sikuku za kiyahudi za kalenda ya kibibilia. Nataka kurejelea kile ambacho mtume Paulo alisema katika 1. Wathesalonike 5:1-4 wakati alisema yafuatayo. "Kuhusiana na wakati na majira, wa pendwa sistahili kuwaandikieni, kwa sababu nyinyi mwalijua kikamilifu kuwa siku ya Bwana yaja kama mwivi ajaye usiku. Kwa kuwa wakati watasema amani na salama ndipo mara kwa gafla uharibifu wa

wajia kama utungu wa mwanamke apataye mtoto; na hawatapotea. Lakini nyinyi wapendwa sio wa giza kuwa siku hiyo iwapate kama mwizi." Paulo alikuwa myahudi na hivyo alielewa ishara za nyakati ambazo zitakua zikifanyika katika wakati na majira ama, sikukuu za wayahudi. Katika kifungu hicho Paulo anahashiria ishara ya amani na salama na anamweleza msomaji kuwa hatakua kwenye giza kwa kuwa atakua akitazama matukio yanayofanyika katika msimu wa sikukuu za kiyahudi. Unapo soma mwanzo 1:14 tunaona jina majira ambalo ni jina la kiibrania kumaanisha wakati ulio teuliwa. Majira, wakati ulio teuliwa, Paulo alikua ana hashiria siku kamili Yesu atakapo rudi katika sikukuu ya tarumbeta ambayo itafanyika katika msimu wa mwanguko wa matawi. Kwa hivyo Paulo aliwambia wayahudi hamna haja niwaandikieni, kua wayahudi waliweza kuelewa kile ambacho Paulo alikuwa anaongea kuhusu. Watu wa pekee ambao watakua kwenye giza wakati Yesu atarudi katika sikukuu watakua wale ambao hawana ufahamu wa neno la Mungu ndani yao. Na hawana ufahamu wa mambo haya ya kibibilia. Tafathali tambua katika ufunuo 3:3, sehemu ya mstari huu, Yesu analiambia kanisa la sardi ambalo lilionekana kuwa kama kanisa lililo kufa kutubu kutokana na njia zao na kutazama. Tambua nini kinacho fanyika wakati unatazama. Na nukuu mtari wa tatu. " **nitakuja kama mwivi wala hutajua saa nitakayokuja kwako".** usisahau Yesu alikuwa anaongoea kuhusu kanisa lililo kufa. Yesu anatuonyesha nini katika kifungu hiki? Kristo anatuonyesha anakuja kama mwizi kwa kanisa lililo kufa na sio kwa kanisa lililo hai. Hawawezi patwa kwa gafla.

Katika ufunuo 3:17-18 Yesu anaongelesha kanisa la Laodicea. Hili ni Kanisa lingine ambalo haliyuko tayari. Yesu analiita vuguvugu. Nini linalo fanyika kwa kanisa vuguvugu? Yesu anatupa jibu katika ufunuo 3:16 wakati anasema **"Hivyo kwa kuwa u uvuguvugu, kwamba wewe si baridi wala si moto, nitakutapika utoke kinywani Mwangu "** tambua katika mistari hii Yesu anawaambia waende wanunue vazi jeupe ili waweze kuvikwa na ilikwamba aibu ya uchi wao ipotee. Kile ambacho watu wengi hawaelewi nikuwa ili vazi jeupe la maanisha nini kimantiki. Kaa nami na utaelewa kwa hakika ni nini. Ufunuo 3:18 ni ufunguo mwingine wa kuelewa anacho tuonyesha Yesu. Na nukuu **18 Kwa hiyo nakushauri ununue kutoka Kwangu dhahabu iliyosafishwa kwa moto ili upate kuwa tajiri na mavazi meupe ili uyavae, upate kuficha aibu ya uchi wako na mafuta ya kupaka macho yako ili upate kuona .**

Nataka ufungamanishe kilicho andikwa ufunuo 16:15 kwa kuunganisha na kifungu Ufunuo 3:18. Hili litakuwa wazi kwako kwa nini ufanye ungamano huo. Ufunuo 16:15 unasema yafuatayo. **15“Tazama, naja kama mwivi! Amebarikiwa yeye akeshaye na kuziweka tayari nguo zake ili asiende uchi na kuoenekana aibu yake”.**

Wacha turejelee tamaduni za kiyahudi kwa sekunde tuu, na ntakuonyesha vile mambo haya yote yanaungamana. Wakati hekalu la kiyahudi lilipo kuwa limesimama wakati Yesu alikua hapa mara ya kwanza Kuhani mkuu na mkuu wa walinzi walikuwa wanajulikana kama 'wezi wajao usiku.' na hili ndilo sababu. Kulikuwa na minara ya kutazama katika hekalu pale ambapo kuhani angalikua akitazama. Jambo moja ambalo alikua atazame ilikua moto katika madhabahu hutazimika. Huu ulikuwa moto wa kiungu ambao uliangukia madhabahu na Mungu aliamurisha moto huu usiwahi zimika. Kuhani alitakiwa kutazama moto huu. Iwapo kuhani angalipatikana akilala wakati mkuu wa walinzi alipokua akizuru, mkuu wa walinzi angechukua kurunzi yake, ambayo ilikuwa karibu na moto wa madhabahu na kuchoma

vazi la kuhani na Kurunzi hiyo. Kuhani angaliamushwa na mwoto, angaliamka na kukimbia kwenye hekalu huku akirarua mavazi yake yaliyokuwa yakiteketea na aibu ya uchi wake ungalionekana.

Sasa waona ufunuo 16:15 wafungamana na yale Yesu alisema kuhusu kanisa lililo kuwa lime kufa. Ukirejelea 1. Wathesalonike 5:1-4 Paulo anasema yafuatayo. **2 kwa kuwa mnajua vema kwamba siku ya Bwana itakuja kama mwivi ajapo usiku** Sasa watambua nini ambacho msemo "**Kama mwivi ajaye usiku**" inamaanisha. Kwa maneno mengine, wakati Yesu atarudi na akupate kama umelala kama yule kuhani hekaluni na kukosa kutizama utahishia kuwa kama yule kuhani, kukimbia na uchi wako na aibu kwa sababu haukuwa tayari kwa mtembeleo wake.

Sasa wacha tutazame Mathayo 25:1-13. Katika vifungu hivi Yesu anazungumzia makundi mawili ya mabikira. Kundi mojo lilikuwa tayari kutazama walikuwa wamejitayarisha kwa ajili ya kuja kwa bwana harusi. Hii ni taswira ya kanisa linalo fanya mapenzi ya Baba, hili nalo linaunganisha harusi ya kiyahudi kwa kuweka mtazamo na kurudi kwa Bwana kuchukua mchumba wake. Yesu alisema bikira watano walikuwa tayari na walikuwa na mafuta kwenye taa zao wakati bwana harusi alikuja. Tambua kuwa Bwana harusi alikuja usiku wa manane kama ilivyo tamaduni. Mabikira watano waliokuwa tayari walienda na Bwana harusi na mlango ukafungwa. Hili litafanyika katika unyakuzi wa kanisa ambao tunaamini utafanyika katika sikuku ya tarumbeta ya wayahudi. Hii ndiyo sababu ni muhimu kutazama kila wakati haswa sana wakati wa sikuku za kiyahudi.

Na jee bikira wale wengine watano ambao hawakua tayari kumlaki Bwana harusi wakati alikuja usiku wa manane? Yesu anatuaharifu kuwa hawakujitayarisha. Hao bikira watano hawakuwa na mafuta kwenye taa zao wakati alikuja usiku wa manane iliwalazimu kwenda kununua ili waangaze njia. Hata hivyo, wakati walirejea mlangoni mwa bwan harusi mlango ulikuwa umefungwa na bwana akasema. "Hakika nawaambieni siwajui." Hii ni taswira ya watu wote ambao hawakuwa wanatazama na wanafungiwa nje ya mlago na Yesu Kristo. Hao bikira watano ambao hawakujitayarisha ni picha ya watu wote ambao watajipata kwenye miaka saba ya dhiki, kwa sababu kama kuhani wa hekalu walikuwa wamelala. Ni kama yule kuhani ambaye alipatwa na mkuu wa walinzi ambaye alijulikana kama mwizi ajaye usiku, ama katika hali hii Yesu Kristo. Kama matokeo yako wewe kutokuwa tayari kama yule kuhani, utapatwa uchi na kwa aibu.

Sasa angalia ujumbe aliyopeana Yesu kuhusu watumishi wema na waovu katika kitabu cha Luka 12:37-40. Huu ndio ujumbe kwa watumishi wema. **37 Heri wale watumishi ambao bwana wao atakapokuja atawakuta wakiwa wanakesha. Amin, nawaambia, atajifunga mkanda wake na kuwaketisha ili wale, naye atakuja na kuwahudumia. 38Itakuwa heri kwa watumwa hao ikiwa bwana wao atakapokuja atawakuta wamekesha hata kama atakuja mnamo usiku wa manane, au karibu na mapambazuko. 39Lakini fahamuni jambo hili kwamba: Kama mwenye nyumba angalijua ni saa ipi mwivi atakapo kuja, asingaliacha nyumba yake kuvunjwa. 40Ninyi nanyi imewapasa kuwa tayari saa zote, kwa maana Mwana wa Adamu atakuja saa ambayo hamumtarajii."**

Katika luka 12:41-47, Yesu anaongea kuhusu watumishi waovu ambao hawakuwa wanafanya mapenzi ya baba, hawakuwa wanamtazamia mwizi usiku. Angalia alicho sema kwa watumishi hawa waovu. **46 bwana wake yule mtumwa atakuja siku asiyodhani, na saa asiyoijua. Huyo bwana wake atamkata vipande**

**vipande na kumwekea fungu lake pamoja nawasio waaminifu. wale** Hawa dio watu waliotambua vyema, walijua mapenzi ya Bwana lakini hawakuwa wakitenda mapenzi yake.

Mstari unaofuata wa 37 unatuambia na huyo mtumishi ambaye alijua mapenzi ya Bwana na hakujitayarisha mwenyewe wala kutenda kulingana na mapenzi yake atachapwa mijeledi mingi. Nakuuliza sasa, je we ni mmoja wajiitao waamini na ila hali hawaki ndani ya Kristo leo, na hawafanyi mapenzi ya Baba? Tunajia kwa hakika kuwa kuna mamilioni ya watu ulimwenguni kote ambao wanajiita wakristo na kwa hakika hawafanyi mapenzi ya Baba. Hiki kikundi cha wakristo hakifanyi mapenzi ya Baba wala hakitazamii kurudi kwa bwana kama vile Yesu aliwaamuru kufanya. Hao watu ambao tunaambiwa walijua mapenzi yake lakini hawakufwata mapenzi yake.

Luka 12:41 Petero anauliza Yesu "Je unapeana huu mfano kwetu ama kwa wote?" Swali hii linaenda kwenye lindi la swali ni nani mtumishi muovu. Yesu akamjibu Petero kwa kumuambia yule mtumshi muovu ni yule asiyefanya mapenzi ya Baba. Mara tena tunaona makundi ya watu yakigawanyishwa mara mbili. Kwanza kulikuwa na bikira kumi, watano walikuwa werevu na tayari na wale wengine tano ambao walikuwa hawamo tayari wakati yesu alikuja usiku wa manane. Sasa tunaona watumishi wema wakitazama na kufanya mapenzi ya Baba ambao watabarikiwa, tukilinganisha na wale wengine waovu ambao wanajua mapenzi ya Mungu lakini hawayatendi wala kutazama na watachapwa.

Jambo lingine la muhimu kukumbuka kuhusiana an sikukuu ya tarumbeta ni hili. Hakuna mtu yeyote ajuaye siku wala saa kwa kuwa siku kuu ya tarumbeta huanza kwa kuonekana kwa mwezi. Wacha nifafanue. Tarehe 30 kila mwezi wanachama wa koti kuu hukusanyika katika malango ya nje ya Yerusalemu pale ambapo hungoja kupokea ushuhuda wa mashahidi wawili wa kuaminika. Mashahidi hawa wawili wanaweza kuhafiki kuwa wameona mwezi.

Punde tu mbalamwezi inapoenekana ingewaruhusu wanachama wa koti kuu kuitakasa mbalamwezi hii ili ashiria kuwa sikukuu ya tarumbeta kuanza.Kwa kawaida ni vigumu mno na kuona mwezi kwa siku ya kwanza kwa vile huonekana tu wakati wa machweo,karibu na jua,wakati laelekea kazkazini.Hivyo basi wao hutazamia upeo mdogo wa mwezi ambao huwa karibu sana na jua na huwa vigumu sana kuonekana.Iwapo upeo huu wa mwezi hungeonekana ifikapo terehe thelathini ya kila mwezi,mbalamwezi ingesherekewa tarehe thelathini na moja.Kwasababu hii sikukuu ya tarumbeta husherekewa siku mbili.Siku hizi mbilli huadhimishwa kama siku moja yenye saa arobaini na nane.sababu ya kuadhinishwa kwa siku mbili ni kuwa iwapo wange subiri kuanza madhimisho punde tu mbalamwezi inapotakaswa,wangekosa nusu ya maadhimisho kwa sababu mbalamwezi waweza tu kutakaswa kipindi cha massa ya mchana.Basi amri yaonekana kuwa vile tuajua majira kaa alivyo sema paulo laikini si siku ama saa jinnsi tulivyoona mathayo 24:32-36.

Yom Teruah ama sikukuu ya tarumbeta ni shererehe pekee ya kiyahudi ambayo siku yake ya kuadhimishwa haijulikani kwa vile hatuna hakika kipindi ambacho mbalamwezi utaonekana.Hivyo basi lazima tuwe macho kuitazamia.Yesu anaposema ya kwamba siku wala saa haijulikani jinsi ilivyo nakiliwa katika mathayo 24:36.anatuambia kuwa ni sikukuu ya tarumbeta pekee ambayo wayahudi hawatambui siku wala saa,ikiambatana na kutokea kwa mbalamwezi.Hivyo basi uadhimisho wa siku mbili.Hakuna

yeyote leo anaweza kukuambia ni lini unyakuzi wa kanisa waweza tokea kwa sababu yaweza kufanyika kwa wakati wowote katika kipindi cha masaa arobaini na nane.

Katika sikukuu ya tarumbeta yesu atarejea kutoa mchumba wake kanisa,na hailipita kanisa linalo fanya mapenzi ya baba,kanisa hili litakuwa liko macho kwa bwana wake kurejeapaulo anaongea kuhusu unyakuzi huu katika 1 wakorintho 15:5-53 pale anaposema,**51Sikilizeni, nawaambia siri: Sote
hatutalala, lakini sote tutabadilishwa 52ghafla, kufumba na kufumbua, parapanda ya
mwisho itakapolia. Kwa kuwa parapanda italia, nao wafu watafufuliwa na miili
isiyoharibika, nasi tutabadilishwa. 53Kwa maana mwili huu wa kuharibika lazima uvae
kutokuharibika, nao huu wa kufa lazima uvae kutokufa.**

Muda fulani katika siku sijazo Yesu akuja toka mbinguni na kuita bi harusi wake,kama ilivyo katika harusi ya kiyahudi.wale ambao tuko macho,bi harusi wake,tutabadilishwa kutoka hii miili ya kiutu na kuvikwa ya kimbinguni.Swali unalopasa kujiuliza ni kuwa Yesu amekuweka wapi?Wewe umiongoni wa wale bikra tano wenye hekima ambao wako tayari kukutana na Bwana?Je,wewe uko imara ukitazamia kurudi kwake?Ama wewe ni mmojawapo wa wale ambao hawako tayari na hawana mafuta ndani ya taa zao?Wewe ni miongoni mwa wale watumishi ambao wakati Yesu anaporudi atakupata unasimama mlangoni ukingoja Bwana kurudi?Ama wewe ni yule mtumishi muovu ambaye anajiita mkristo lakini hafanya mapenzi ya baba,wale ambao watahesabiwa na wasioamini wakati Bwana atarudi kumchukua bi harusi wake.Amka kanisa na uchague ni upande upi utakua,mwanga ama giza.kama wewe si mkristo nasema amka kwa kila Yesu amekuonyesha na utubu ili uhesabiwe haki ya kuponyoka mambo haya yote na usimame mbele ya mwana wa adamu,Yesu kristo.


## 2011 Tarehe za sikukuu za kibibilia za kiyahudi

sikukuu ya tarumbeta(Yom Teruah/Rosh Hashanah),machweo ya septemba 28 hadi mwaliko wa usiku septemba 30

siku ya kuondolewa thambi(Yom Kippurim) machweo ya octoba 7 hadi mwaliko wausiku wa octoba 8

sikukuu ya hema(sukkot)machweo ya octoba 12 hadi mwaliko wa usiku wa octoba 19.

Kuna sikukuu 7 sa kiyahudi.Za kwanza nne hufanyika majira ya kwanza.hizi sikukuu za majira ya kwanza zilitimika.zilitimika wakati Yesu kristo alikuja duniani kwa mara ya kwanza.Naamini kuwa zifuatazo ytayu zitatimika katika sokukuu inayoungamanishwa na kurudi kwake kwa mara ya pili.sikukuu itakoyo fuata kutimika kupitia kwa Yesu ni nambari tano.tazama mchoro hapa chini.




Jinsi Yesu alitimiza karamu za kwanza nne

ukisoma kutoka 12:1-6 utaona kuwa wayahudi wangalichagua mwanakondoo and wangalimtazama kwa ukaribu kwa muda wa siku nne kabla kumchinja siku ya pasaka.Yesu alitimiza sehemu hii hadi mwisho,wakati alimpanda mwanapunda na kuingia Yerusalemu.Wakristo huita siku hii jumapili ya matende.Kwa siku nne Yesu alitazamwa kwa karibu na viongozi wa kidini na wale wamamlaka.Yesu alikuwa mwanakondoo bila mawaa!Alitimiza kuwa mwanakondoo aliye chaguliwa Nisan 10,ambao ilikuwa jumamosi,sabato.Alikuja Yerusalemu akiwa amebebwa na mwana punda na kutimiza zekaria 9:9.Matt 21:1-10 anaelezea yesu akiingia yerusalemu.

Wacha tusome kutoka 12:1-6 **BWANA akamwambia Mose na Aroni katika nchi ya Misri,**
**2“Mwezi huu utakuwa mwanzo wa miezi kwenu, yaani, mwezi wa kwanza wa mwaka**
**wenu. 3Iambie jumuiya yote ya Israeli kwamba katika siku ya kumi ya mwezi huu, kila**
**mtu atatwaa mwana kondoo mmoja kwa ajili ya familia yake, mmoja kwa kila nyumba. 4**
**Ikiwa nyumba yo yote ina watu wachache wasioweza kumaliza huyo mwana kondoo**
**mzima, nyumba hiyo itabidi ishirikiane na nyumba ya jirani wa karibu, baada ya**
**kuzingatia idadi ya watu waliomo. Mtaangalia ni kiasi gani cha nyama kitahitajika**
**kulingana na mahitaji ya kila mtu. 5Wanyama mtakaowachagua, lazima wawe wa kiume**
**wa umri wa mwaka mmoja wasio kuwa na dosari, mwaweza kuwachukua kati ya kondoo**
**au mbuzi. 6Tunzeni wanyama hao mpaka siku ya kumi na nne ya mwezi, ambapo lazima**
**watu wa jumuiya yote ya Israeli wachinje wanyama hao wakati wa jioni.**

Bibilia inasema kuwa kristo alikuwa mwanakondoo huu wa dhabihu iliyo kamili,kwa kutimiza maandiko,wakati wa Nisan 10.Mtume Paulo anatueleza mara tatu sehemu tofauti kuwa Yesu alihakikishwa kuwa "mwanakondo wa mungu" ambaye huondoa dhambi za ulimwengu.Soma Yohana 1:**29 29Siku iliyofuata, Yohana alimwona Yesu akimjia akasema, “Tazama, Mwana Kondoo wa Mungu aichukuaye dhambi ya ulimwengu.**

Ufunuo 5:6 **Ndipo nikaona kati ya kile kiti cha enzi na wale viumbe wenye uhai wanne na miongoni mwa wale wazee, Mwana-Kondoo amesimama, akiwa kama amechinjwa. Alikuwa na pembe saba na macho saba, ambazo ndizo zile Roho saba za Mungu zilizotumwa duniani pot**

Ufunuo 7:10 **walikuwa wakipiga kelele kwa sauti kubwa wakisema: "Wokovu una Mungu wetu, Yeye aketiye kwenye kiti cha enzi na Mwana-Kondoo!''**

Huu ndio mfananisho wa kinabii wa sikukuu saba za kilawi za Israeli


1) Pasaka (mambo ya walawii 23:5)- inaonyesha kuwa masihi ndie mwana kondoo wetu wa pasaka (wakorintho wa kwanza 5:7) ambaye damu yake ilimwagika kwa ajili ya dhambi zetu.Yesu alisulubiwasiku ya matayarisho ya pasaka wakati huo huo kondoo wa pasaka walikkuwa wakichinjwa jioni hiyo.

2) Mikate isiyo tiwa chachu (mambo ya walawii 23:6)-inaonyesha maisha ya masihi yasiyo kuwa na dosari(chachu ni ishara ya dhambi katika bibilia) Hii inamfanya awe dhabihu kamili ya dhambi zetu.Mwili wa Yesu ulikaa ndani ya kaburi siku moja ya sikukuu hii,kama ngano iliyo pandwa na kungojea kulimbuka kama mkate wa uzima.

3)malimbuko(mambo ya walawii 23:10)inaonyesha kufufuka kwa masihi kama tunda la uhaki.Yesu alifufuka siku ii hii,ambapo ndio sababu Paulo anamwita kama "tunda la kwanza kutoka kwa wafu"

4)Majuma au pentekoste(mambo ya walawii 23:16) ilifanyika siku hamsini baada ya kuanza kwa sikukuu ya mkate usiotiwa chachu na inaonyesha mavuno kubwa ya roho na kipawa cha Roho mtakatifu kwa wayahudi na mataifa,wale ambao wataletwa kwenye ufalme wa mungu wakati wa nyakati za kanisa.(ona matendo ya mitume 2)Kanisa lilianzishwa siku hiiwakati mungu alimimina roho mtakatifu na wayahudi 3,000 wakakubali mwito wa Petero wakati wa mafundisho yake ya kwanza ya kutangaza habari njema.

YESU ATATIMIZA SIKUKUU ZILIZOSALIA TATU WAKATI WAKURUDI KWAKE MARA YA PILI.ONA 5-7 HAPA CHINI




5)Tarumbeta (mambo ya walawii 23:24) malimbuko ya kwanza ya sikukuu.Wengi huamini kuwa siku hii inaashiria unyakuzi wa kanisa wakati masihi Yesu ataonekana mawinguni akikujia bi harusi wake,kanisa.Unyakuzi huhusishwa na kupuliza kwa sauti tarumbeta.(wathesalonike wa kwanza 4:13-18 na wakorintho 15:52)

6)Siku ya upatanisho.(mambo ya walawii 23:27) wengi huamini kiunabii hii inaonyesha kurudi kwa yesu mara ya pili wakati atarudi hapa duniani.Hiyo iatakuwa siku ya upatanishi kwa masalio wa wayahudi wakati "watamtazama yule waliemdunga kwa mkuki,"watubu dhambi zao na kumpokea kama masihi.(zakaria12:10 na warumi11:1-6,25-36)

7)hema ama vibanda (mambo ya walawii 23:34) Wasomi wengi wanaamini kuwa sikukuu hii inaonyesha ahadi ya Bwana kuwa mara tena atashirika na watu wake wakati atarudi kutawala ulimwengu (mika 4:1-7).Kama nilivyo sema  hakuna  anaweza kujua kama kurejelea kujenga kwa waisraeli kutaalika vita vingine ambavyo vya weza kuwa unabii wa mwisho hizi siku za mwisho.Kama PLO watavamia Israeli kwa sababu ya kurejelea kujenga katika kile wanaita ardhi yao tunaeza ona vita vya zaburi 83 vikizuka.Na nani ajuaye kuwa tunaweza nyakuliwa kipindi hiki? Yesu pekee ndiye ajuaye na naweza kuambia,nitakuwa tayari wakati wowote atuitapo nyumbani.Je, wewe?Wacha nirejelee wito wa usalama na amani.

Hakuna yeyote anayepaswa kupatikana kwa giza kama mwizi usiku.makinika katika sikukuu hizi za mwanguko na uwe tayari haswa sana wakati wa sikukuu ya tarumbeta,kama tujuavyo kuja kwa Bwana kuchukua bi harusi wake si mbali na sasa.